

Swahili

# Msaada wa Mtoa Huduma kwa Familia

Huduma za Jamii Manispaa ya Bollnäs

## **MTUJI**

Manispaa ya Bollnäs

Kituo cha Huduma za Jamii (Socialförvaltningen)

Simu: 0278-257 15

Baruapepe: [anhorigstod@bollnas.se](mailto:anhorigstod@bollnas.se)

Anuani ya kutembelea: Våggatan 11

Anuani ya Posta 82142 Bollnäs

[www.bollnas.se/anhorigstod](http://www.bollnas.se/anhorigstod)



## Msaada wa Mtoa Huduma kwa Familia katika Bollnäs

Msaada wa Mtoa Huduma kwa Familia unahusika na hatua tofauti ambazo zimelenga kufanya mambo yawe rahisi kwa watu ambao wanahitaji msaada katika maisha yao ya kila siku, iwe ni kutokana na ugonjwa, ulemavu, matumizi ya madawa, matatizo ya kimahusiano yanayotokana na umri mkubwa/kuzeeka. Unaweza kuficha jina lako, na tuna wajibu wa kutunza siri. Msaada wa mtoa huduma kwa familia upo kwa ndugu wote, bila kujali umri, na hauhitaji kuwa na jitihada zingine katika huduma za jamii ili kutumia msaada wa mtoa huduma kwa familia

## Maelezo ya mawasiliano

Namba ya simu kwa ajili ya msaada wa mtoa huduma kwa familia ni **0278- 25715**.

Baruapepe ni: [anhorigstod@bollnas.se](mailto:anhorigstod@bollnas.se)

## Pumziko

Ikiwa wahitaji kupumzika kutoka katika kazi za mtoa huduma, tunaweza kutoa pumziko hilo. Pumziko linaweza kutolewa nyumbani kwako au katika nyumba zetu wenyewe zilizo salama na za kuliwaza zilizopo Våggatan 11. Pumziko ni la bure, na una hiari kulipata hadi kwa saa 20 kwa mwezi. Ikiwa ndugu zako wanapata huduma katika majengo salama, gharama ya chakula haitozwi.

## Kituo cha huduma ya kila siku

Kituo cha huduma ya kila siku kinatoa fursa kwa watoa huduma wa familia kupumzishwa kutoka kwenye kazi zao kwa muda wakati ambapo ndugu zao wanakuwa na siku nzuri ya kufurahia pamoja na wengine. Kituo cha huduma ya kila siku kinatumia mbinu ya kuwarudisha katika hali zao, na lengo kuu likiwa kuwapa wagonjwa wote siku nzuri ya raha na yenye kufurahisha. Kituo cha huduma ya kila siku kipo katika majengo ya mtoa huduma wa familia katika Våggatan 11.

## Vikundi vya Watoa huduma

Vikundi vya watoa vinakupa fursa kukutana na watoa huduma wengine ambao wapo katika hali sawa kama wewe mwenyewe. Wanatoa fursa kubadilisha uzoefu, wasiwasi na maneno ya kutia moyo na watoa huduma wengine. Kufanya vitu pamoja, kujifunza pamoja na kupokea taarifa

## Kukaa kwa muda mfupi mara kwa mara

Dhumuni la kukaa kwa muda fupi mara kwa mara ni kufanya mambo yawe rahisi kwa mtu mwenye anayehitaji huduma kuendelea kuishi nyumba na kutoa pumziko/nafuu kwa mtoa huduma wa familia yake. Nafasi kwa ajili ya kukaa kwa muda mfupi mara kwa mara zinapatikana Ängslunda. Ili kuomba nafasi ya kukaa kwa muda mfupi mara kwa mara, wasiliana na msimamizi wako wa huduma kwa namba 0278-250 00

## Mshauri wetu wa Huduma ya familia Åsa Svärd anaweza kutoa

- Ushauri na msaada kwa matatizo yanayohusiana na huduma ya familia
  - Mazungumzo ya ana kwa ana ambapo utapata fursa kuelezea mawazo na hisia zako kuhusu hali yako katika mazingira tulivu yaliyotulia.
  - Ziara za nyumbani
- Unaweza kumpata mshauri wa huduma ya familia kwa kupiga namba 0278-25716

## Muuguzi wetu wa ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu Marianne Sundström anaweza kutoa

- ushauri
- Mazungumzo ya ana kwa ana
- Ziara za nyumbani au ahadi za kukutana zikihitajika
- Wasiliana na watoa huduma za afya

Unaweza kumpata muuguzi wa ugonjwa wa kupoteza kumbukumbu kwa kupiga simu namba 0278-253 08